
JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO

# BAJETI TOLEO LA WANANCHI




**BAJETI YA SERIKALI YA MWAKA 2017/18 KWA LUGHA RAHISI**

Imetolewa na Wizara ya Fedha na Mipango

policy forum

Kwa kushirikiana na Policy Forum

## 1. UTANGULIZI

Bajeti ya Serikali toleo hili la Wananchi linatoa muhtasari kuhusu bajeti ya Serikali kwa mwaka 2017/18. Kijitabu hiki kina maeneo muhimu sita, ambapo eneo la kwanza ni utangulizi unaoelezea dhana ya bajeti na bajeti ya wananchi pamoja na malengo ya bajeti ya mwaka 2017/18. Maeneo yanayofuata yanahusu: Misingi na shabaha ya uchumi jumla; Vipaumbele vya bajeti ya mwaka 2017/18; Sera na hatua za kuiwezesha bajeti ya 2017/18; Vyanzo vya mapato na kiasi chake; na Matumizi mbalimbali yanayotarajiwa

### *Bajeti ya Serikali ni nini?*

Ni mpango wa Serikali unaoelezea jinsi mapato yanavyopatikana na jinsi Serikali itakavyotumia mapato hayo kwa kipindi cha mwaka mmoja wa fedha. Kimsingi, ni nyenzo muhimu kinachotumiwa na Serikali kutafsiri sera zake na kuanisha gharama zitakazotumika na hivyo kusaidia kugawa rasilimali zilizopo ili kutekeleza sera na vipaumbele vya taifa katika muda kati.

### *Bajeti ya Wananchi*

Kila mwaka, Serikali huandaa bajeti na kuwaisilisha Bungeni ili iweze kujadiliwa na kuidhinishwa. Kwa kawaida, bajeti ya mwaka inayowasilishwa huwa ni ndefu na imeandikwa kwa lugha ya kitaalam na pia huambatana na viambatisho na nyaraka mbalimbali. Kwa sababu hiyo, **Bajeti ya Wananchi** huandaliwa ili kuwasilisha bajeti ya Serikali kwa Wananchi kwa lugha rahisi na inayoeleweka kwa wote. Hii ni moja ya hatua za Serikali kw mfululizo sasa kuwapa wanachi taarifa ya bajeti ya nchi. Lengo ikiwa n ya kushiriki katika mipango na mchakato wa bajeti.

policy forum

### *Malengo ya vaka 2017/18*

Bajeti ya mwaka 2017/18 ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/17 - 2020/21) ikiwa na lengo la kuchochea mapinduzi ya viwanda na maendeleo ya watu. Hatua zilizopendekezwa katika bajeti ya 2017/18 zina lengo la kujenga misingi imara ya kiuchumi kwa ajili ya uchumi wa viwanda na kupanua fursa za ajira pamoja na biashara chini ya kauli mbiu: "**Kujenga uchumi wa viwanda utakaochochea ajira na ustawi endelevu wa jamii"** Hii itasaidia kufikia Dira ya Taifa ya kufikia uchumi wa kipato cha kati ifikapo 2025.

## 2. MISINGI NA SHABAHA YA SERA ZA UCHUMI JUMLA

Bajeti ya mwaka 2017/18 inalenga kufikia malengo ya uchumi jumla yafuatayo:

a. Pato la Taifa kukua kwa asilimia 7.1 mwaka 2017 kutoka asilimia 7.0 mwaka 2016;
b. Kiwango cha mfumuko wa bei kutengemaa katika wigo tarakimu moja, kwa wastani wa asilimia kati ya 5.0 hadi 8.0 mwaka 2017;
c. Mapato ya ndani yakijumuisha vyanzo vya Mamlaka za Serikali za Mitaa (Halmashauri) yaweze kufikia asilimia 16.5 ya pato la taifa mwaka 2017/18 kutoka asilimia 15.8 mwaka 2016/17;
d. Kuongeza mapato ya kodi kufikia asilimia 14.2 ya Pato la Taifa mwaka 2017/18 kutoka asilimia 13.3 mwaka 2016/17;
e. Matumizi kwa ujumla wake yaweze kufikia asilimia 26.2 ya Pato la Taifa mwaka 2017/18 kutoka asilimia 23.7 mwaka 2016/17;
f. Kupunguza nakisi ya bajeti hadi asilimia 3.8 ya Pato la Taifa mwaka 2017/18 kutoka asilimia 4.5 mwaka 2016/17; na
g. Akiba ya fedha za kigeni yenye kukidhi uingizaji wa bidhaa za nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne, ifikapo June 2018.

Ili kufikia malengo yaliyokusudiwa, misingi ifuatayo inatakiwa kuzingatiwa na kudumishwa:

a. Amani, umoja, utulivu wa kisiasa ndani ya nchi na katika kanda;
b. Kutengemaa na uendelevu wa viashiria vya uchumi jumla (ikijumuisha ukuaji wa pato la taifa, biashara ya nje, ukusanyaji wa mapato ya ndani);
c. Kutengemaa kwa uchumi wa dunia;
d. Kutengemaa kwa bei za mafuta ya petrol kwenye soko la dunia;
e. Hali nzuri ya hewa nchini na katika nchi za jirani;
f. Uhusiano mzuri na nchi jirani, kikanda na kimataifa; na
g. Kuwepo kwa Sheria na Kanuni wezeshi kwa wawekezaji.

# 3. VIPAUMBELE VYA BAJETI YA SERIKALI 2017/18

## *Maeneo ya vipaumbele Pamoja na Vipaumbele vyake vya Uchumi kwa mwaka 2017/18*

Bajeti ya Serikali ya mwaka 2017/18 ni ya pili katika utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17 - 2020/21). Kwa kuzingatia hilo, bajeti inalenga kutekeleza maeneo muhimu ya Kipaumbele kama yalivyoelezwa kwenye mpango wa maendeleo wa miaka mitano, ambayo ni:

**a. Shunghuli za kuendeleza ukuaji wa uchumi na ujenzi wa viwanda ;**

- ⇨ Kuongeza kasi ya kukuza uchumi ili kufikia uchumi wa kipato cha kati.
- ⇨ Kuweka mkazo kwenye maendeleo ya viwanda huku ikizingatiwa kuwa Sekta Binafsi ndiyo muhimili muhimu katika kujenga uchumi wa viwanda. (Viwanda vinavyolengwa ni vile vya kuzalisha ajira nyingi, vyenye kutumia malighafi ya ndani ya nchi, na vile vya kuzalisha bidhaa ambazo zitatumiwa na watu wengi ndani ya nchi).
- ⇨ Kuboresha mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi kwa kulenga zaidi kwenye kuyaongeza thamani na kuzifanya shughuli za kilimo kuwa za kisasa kwa kutoa mafunzo, pembejeo, zana na wataalamu.
- ⇨ Kuhakikisha kuwa madini na maliasili zetu vinatumika kwa ipasavyo kwa manufaa ya taifa letu.
- ⇨ Kuweka mkazo katika kuendeleza utalii, matumizi ya ardhi na usimamizi wa mazingira.

**b. Kufungamanisha uchumi na maendeleo ya watu;**

- ⇨ Kuongeza ubora wa elimu, huduma za afya, maji na umeme.

**c. Kujenga mazingira wezeshi kwa uendeshaji biashara na uwekezaji;** na

- ⇨ Kuboresha miundombinu ya kiuchumi kama vile barabara, reli, usafiri wa anga na wa majini na umeme.

**d. Kuimarisha usimamizi wa utekelezaji wa Mpango**.

- ⇨ Kuongeza mapato, kuziba mianya ya upotevu wa rasilimali za Serikali, kudhibiti matumizi na kusimamia Sheria ya ununuzi wa umma.
- ⇨ Kupambana na rushwa, ufujaji na matumizi ya madawa ya kulevya.

## *Miradi ya Kipaumbele kwa Mwaka 2017/18*

Hii ni miradi ambayo inaonekana kuwa muhimu na utekelezaji wake unatarajia kutoa matokeo makubwa katika ukuzaji wa uchumi, na kuchochea miradi mingine ya kiuchumi, na hivyo kuielekeza Tanzania kwenye mapinduzi ya viwanda na kuchochea maendeleo ya watu. Sehemu kubwa ya miradi hii ni ile iliyoanzishwa mwaka 2016/17, na kwa hiyo itakuwa ni miradi inayoendelea. Miradi hii ni pamoja na:


a. Ujenzi wa reli mpya ya kati kwa kiwango cha ***standard gauge***;
b. Kufufua Shirika la Ndege Tanzania kwa kununua ndege mpya;
c. Uchimbaji wa makaa ya mawe na chuma na ujenzi wa kiwanda changamano *(complex)* cha chuma cha pua *(steel)* Mchuchuma na Liganga, Njombe;
d. Uanzishwaji wa Kanda Maalum za Kiuchumi (SEZs) ili kukuza uwekezaji, biashara na shughuli za viwanda;
e. Ujenzi wa mtambo wa kusindika gesi asilia kimiminika, Lindi;
f. Ujenzi wa bomba la kusafirisha mafuta ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania);
g. Kupanua miundombinu ya kiuchumi hasa, ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya reli, barabara, madaraja, bandari na viwanja vya ndege;
h. Uboreshaji wa usafiri katika Maziwa Makuu;
i. Kuanzisha shamba la kilimo cha miwa na kiwanda cha sukari, Mkulazi-Morogoro;
j. Kusomesha kwa wingi kwenye fani na ujuzi maalum kwa ajili ya ujenzi wa viwanda, na maendeleo ya watu na pia kuendeleza sayansi, teknolojia na ubunifu.Hii ni pamoja na ukamilishaji wa skuli za udaktari, Mloganzila na Dodoma.

# 4. SERA NA HATUA MUHIMU ZA KUIWEZESHA BAJETI YA MWAKA 2017/18

## *Hatua za Kiutawala kwa uzalishaji Mapato*

Ili kuhakikisha bajeti ya mwaka 2017/18 inatekelezwa ipasavyo, Serikali itaongeza na kuimarisha ukusanyaji wa mapato. Hatua zifuatazo za kiutawala zitarahisisha na kuongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani:

- Kuendelea kuhimiza matumizi ya vifaa vya kiektoniki na mifumo kama vile vifaa vya kieletroniki vya kukusanya mapato (*EFDs*) , Mfumo wa kieletroniki wa ukusanyaji mapato (*e-RCS* ) na mfumo wa kieletroniki wa ukusanyaji wa mapato




ya Serikali (*GEPGS*) ili kudhibiti uvujaji wa mapato.

- Kuendelea kupanua wigo wa kodi ikiwa ni pamoja na kurasimisha sekta isiyo rasmi.
- Kuboresha ufuatiliaji wa makusanyo na kuimarisha usimamizi wa mapato yasiyo ya kodi;
- Kuendelea kufanya uthamini halaiki wa majengo chini ya usimamizi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ili kuongeza mapato yatokanayo na kodi ya majengo.
- Kurasimisha miliki za ardhi kwa lengo la kuongeza mapato.

- ⇨ Kuendelea kuchukua hatua za udhibiti kwa lengo la kupunguza misamaha ya kodi isiyo na tija.
- ⇨ Kuanzisha maeneo ya kuhakiki na kisha kuruhusu madini kusafirishwa nje ya nchi kwenye maeneo ya viwanja vya ndege vya kimataifa, migodini na kwenye maeneo mengine yanayofaa.

## *Mabadiliko ya Sera za Mfumo wa Kodi, Ada, Tozo Na Mapato Mengine*

Katika bajeti ya mwaka 2017/18 Serikali imefanya marekebisho ya mfumo wa kodi ikiwa ni pamoja na viwango vya kodi, ada na tozo zinazotozwa chini ya sheria mbalimbali za kodi. Lengo ni ***kuongeza mapato ya Serikali***, ***kuongeza fursa za ajira*** na ***kuchochea ukuaji wa uchumi*** hasa katika sekta ya viwanda, kilimo na usafirishaji. Maeneo muhimu yaliyofanyiwa marekebisho ni:

a. **Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT), SURA 148** imerekebishwa ili kusamehe kodi kwenye:
  - ⇨ Bidhaa za mtaji (kwa viwanda vya mafuta ya kula, nguo, ngozi, dawa za binadamu na mifugo) ili kuvutia uwekezaji;
  - ⇨ Huduma saidizi za usafirishaji ili kuzifanya huduma za bandari zetu kuwa nafuu na zenye ushindani;
  - ⇨ Vyakula vya mifugo vinavyotengenezwa hapa nchini na mayai ya kutotolesha vifaranga ili kupunguza gharama za uzalishaji kwa wakulima.

b. **Sheria ya Kodi ya Mapato, SURA 332** imerekebishwa ili:
  - ⇨ Kurekebisha muda wa kutoza kodi mbadala kwa makampuni yanayopata hasara kuwa miaka mitatu mfululizo badala ya miaka mitano;
  - ⇨ Kuongeza kiwango cha juu kinachotumika kama gharama ya kukokotoa uchakavu wa magari yasiyo ya kibiashara kutoka shilingi milioni 15 hadi shilingi milioni 30;
  - ⇨ Kupunguza Kodi ya Mapato ya Makampuni kutoka asilimia 30 mpaka asilimia 10 kwa miaka mitano ya mwanzo tangu kuanza uzalishaji kwa waunganishaji wa magari, matrekta na boti za uvuvi, kuhamasisha uhaulishaji wa teknolojia na kuongeza ajira;
  - ⇨ Kuanza kutoza kodi ya Zuio ya mwisho kwa wachimbaji wadogo wadogo wa madini kwa kiwango cha asilimia 5 kwenye bei ya kuuzia ili kupata mapato stahiki kutoka sekta ya madini.

c. **Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, SURA 147** imerekebishwa ili:
  - ⇨ Kurekebisha kulingana na mfumo wa viwango maalum vya ushuru vinavyotozwa kwenye bidhaa zisizo za petroli kwa kiwango cha asilimia 5. Marekebisho haya hayahusishi baadhi ya bidhaa zinazozalishwa ndani ili

kuunga mkono Mkakati wa taifa wa kujenga uchumi wa viwanda. Marekebisho yatahusisha: vinywaji baridi, maji yanayozalishwa nje, juisi ya matunda, bia, vinywaji vingine visivyo na kilevi, mvinyo, pombe kali na sigara.

⇨ Kufuta Ada ya Mwaka ya Leseni ya Magari na kuongeza ushuru wa bidhaa kwenye mafuta ya petroli, dizeli na taa kwa shilingi 40 kwa lita ili kufidia mapato yatokanayo na kusitishwa kwa ada ya leseni ya magari kila mwaka.




d. **Sheria ya Usalama Barabarani, SURA, 168** imerekebishwa ili kufuta Ada ya Leseni ya Magari kwa kila mwaka, ili ada hiyo ilipwe mara moja tu wakati wa usajili wa gari. Aidha, msamaha wa kodi umetolewa kwa ada za leseni za magari yote ambayo yalikuwa hayajalipiwa huko nyuma. Ada ya Leseni ya Magari wakati wa usajili wa mara ya kwanza itakuwa kama ifuatavyo:

| Ujazo wa Injini (CC) | Kiwango kilichokuwa Kinalipwa (Sh) | Kiwango Kitakacholipwa Sasa (Sh) | Ongezeko (Sh) |
|---|---|---|---|
| **501 - 1500** | 150,000/= | 200,000/= | 50,000/= |
| **1501 - 2500** | 200,000/= | 250,000/= | 50,000/= |
| **2501 na Zaidi** | 250,000/= | 300,000/= | 50,000/= |

e. **Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, SURA 290** imerekebishwa ili kupunguza Ushuru wa Mazao unaotozwa na Mamlaka za Serikali za mitaa kutoka asilimia tano (5) hadi asilimia tatu (3) kwa mazao ya biashara; na kutoka asilimia tano (5) hadi asilimia mbili (2) kwa mazao ya chakula. Aidha, mtu anayesafirisha mazao yake kutoka Halmashauri moja kwenda nyingine yasiyozidi tani moja (1) hatatozwa Ushuru huu.
f. **Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004** imerekebishwa ili kufanya mapitio ya kina ya viwango vya Ushuru wa Pamoja wa Forodha; na kufanya marekebisho ya Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, ya mwaka 2004 katika mwaka wa Fedha 2017/18.
g. **Marekebisho ya Viwango vya Ada na Tozo Mbalimbali** zinazotozwa na Wizara, Idara zinazojitegemea na Mikoa kwa kufuta:
   - ⇨ Ada ya ukaguzi wa viwango, Ada ya Ukaguzi wa Mionzi na Ada ya Uzani wa Vipimo kwenye mbolea, ada ya ukaguzi wa ubora wa mazao ya biashara kama vile pamba, chai, korosho na kahawa.
   - ⇨ Ushuru wa Huduma kwenye nyumba za kulala wageni zinazotoza tozo la nyumba za wageni;
   - ⇨ Ushuru wa Mabango kwa mabango yanayoelekeza mahali huduma za umma zinapopatikana kama vile shule, hospitali au zahanati;
   - ⇨ Ada ya vibali vinavyotolewa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya shughuli mbalimbali;
   - ⇨ Ada mbalimbali zinazotozwa mifugo kwenye minada.

## *Hatua muhimu za kudhibiti Matumizi*

Serikali itaendelea kudumisha nidhamu ya fedha ili kupata thamani ya fedha. Katika kufikia azma hiyo, Serikali itafanya yafuatayo:

a. Kuhakikisha kuwa mashirika ya umma ya kibiashara, yanaendeshwa kwa faida bila kutegemea ruzuku ya Serikali.
b. Kuhakikisha kwamba mikataba yote inayoingiwa na Serikali na Taasisi zake inakuwa katika shilingi za kitanzania isipokuwa kwa mikataba inayohusisha biashara na huduma za kimataifa ili kujikinga na vihatarishi vya kifedha kwa kutumia teknolojia banifu.
c. Kuendelea kudhibiti matumizi ya huduma za umeme, simu na maji kwenye ofisi za umma;
d. Kuendelea kudhibiti ulipaji wa mishahara kwa kulipa watumishi wanaostahili;
e. Kusisitiza matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika kufanikisha mawasiliano kwenye shughuli za Serikali.
f. Kuthibiti malimbikizo ya madeni.

## 5. NI KWA JINSI GANI SERIKALI INAPATA FEDHA?


Katika mwaka 2017/18 Serikali ina lengo la kukusanya **Shilingi bilioni 31,712.0** ili zitumike kuendesha shughuli zake na kutimiza mipango yake. Mapato hayo yanatarajiwa kutoka kwenye vyanzo vifuatavyo:

a. **Shilingi bilioni 17,106.3** kutoka kwenye **Kodi** ikijumuisha; *Kodi ya Mapato* (kutokana na mishahara, vipato vya watu binafsi na makampuni); *Kodi ya Ongezeko la Thamani na Ushuru wa bidhaa* (kwenye ununuzi wa bidhaa na huduma); na *Ushuru wa Forodha na bidhaa zinazouzwa nje* (kwenye uagizaji na usafirishaji wa bidhaa nje).

b. **Shilingi bilioni 2,870.7** kutoka kwenye **Mapato Yasiyo ya Kodi** ikijumuisha; faini, ada, uuzaji wa nyaraka za zabuni na mapato ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

c. **Shilingi bilioni 3,967.1** kutoka kwenye **Misaada na Mikopo Nafuu** ikijumuisha Misaada ya Kibajeti, Misaada na Mikopo Nafuu ya Miradi na ya Kisekta.

d. **Shilingi bilioni 7,763.9** kutoka kwenye **Mikopo ya Ndani na Nje** ikijumuisha; mikopo ya masharti ya kibiashara ya ndani na nje ya nchi ambayo ni asilimia moja (1) ya Pato la Taifa




## 6. JINSI SERIKALI INAVYOTARAJIA KUTUMIA MAPATO YAKE

Serikali inatarajia kutumia **Shilingi bilioni 31,712.0** katika shughuli zake zilizopangwa kutekelezwa mwaka 2017/18. Matumizi ya Serikali yatafanyika yakiwa yamegawanywa kwenye makundi makuu mawili kama ifuatavyo:

a) **Matumizi ya Kawaida** kwa ajili ya shughuli za uendeshaji kama vile kulipa mishahara na marupurupu kwa watumishi wa umma, mahitaji ya ofisi na huduma mbalimbali, riba kwenye deni la taifa, matengenezo na ukarabati wa nyenzo na vifaa. Serikali imepanga kutumia Jumla ya **Shilingi bilioni 19,712.4** kwa matumizi ya kawaida.

b) **Matumizi ya Maendeleo** kugharamia miradi ya maendeleo kama vile ujenzi wa barabara, shule, hospitali, miundombinu ya maji na ununuzi wa rasilimali mpya. Jumla ya **Shilingi bilioni 11,999.6** zitatumika kwa matumizi ya maendeleo.




### *Fedha zinazopelekwa kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa*

Serikali inatarajia kupeleka **shilingi bilioni 5,831.8** kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa kama ruzuku. Kati ya hizo **shilingi bilioni 4,541.1** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na

**shilingi bilioni 1,290.7** ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Fedha zinazopelekwa kwenye Mamlaka hizo zitatumika kuboresha utoaji wa huduma kwenye Serikali za Mitaa katika sekta zifuatazo:


| Sekta | Matumizi ya Maendeleo (Shilingi) | Matumizi ya Kawaida (Shilingi) | Jumla ya Matumizi (Shilingi) |
|---|---|---|---|
| **Kilimo** | Bilioni 139.1 | | Bilioni 139.1 |
| **Afya** | Bilioni 669.79 | Bilioni 112.09 | Bilioni 781.88 |
| **Barabara** | Bilioni 33.88 | Bilioni 170.22 | Bilioni 204.1 |
| **Maji** | Bilioni 25.54 | Bilioni 70.44 | Bilioni 95.98 |
| **Elimu** | Bilioni 3,024.58 | Bilioni 201.66 | Bilioni 3,226.24 |
| **Utawala** | Bilioni 647.98 | Bilioni 736.27 | Bilioni 1,384.25 |
| **Jumla** | **Bilioni 4,541.1** | **Bilioni 1,290.7** | **Bilioni 5,831.8** |

## *Matumizi kulingana na Majukumu ya Serikali*

Kwa mujibu wa majukumu ya Serikali, matumizi kwa nchi nzima yametengwa kama ifuatavyo:

a. **Shilingi bilioni 10,246** ni kwa ajili ya **Huduma za Jumla za Umma** (inajumuisha; huduma za jumla, mihimili ya Dola na Bunge, masuala ya fedha na kibajeti na Hazina, mambo ya nje, na deni la Taifa).
b. **Shilingi bilioni 1, 724** ni kwa ajili ya **Ulinzi na Usalama**.
c. **Shilingi bilioni 916** ni kwa ajili ya **Usimamizi wa Sheria na Usalama wa Raia** (inajumuisha; polisi, magereza, zima moto, ulinzi wa raia, mahakama).
d. **Shilingi bilioni 10,717** ni kwa ajili ya **Masuala ya Kiuchumi** (inajumuisha; Viwanda, biashara, masuala ya ajira, kilimo, uvuvi, madini, nishati, usafirishaji, mawasiliano, misitu, maliasili na utalii).
e. **Shilingi bilioni 100** ni kwa ajili ya **Uhifadhi wa Mazingira.**
f. **Shilingi bilioni 673** ni kwa ajili ya **Makazi na huduma za Jamii** (inajumuisha; makazi, huduma za maji, maendeleo ya jamii).
g. **Shilingi bilioni 2,222.3** ni kwa ajili ya **Afya**.
h. **Shilingi bilioni 23** kwa ajili ya **Burudani, Utamaduni** na **Dini** (inajumuisha; masuala ya vijana, michezo, huduma za utamaduni, utangazaji na huduma za kidini).
i. **Shilingi bilioni 4,706** ni kwa ajili ya **Elimu** (inajumuisha; Elimu ya awali, msingi, sekondari na vyuo; Elimu ya juu; mafunzo ya ufundi stadi na mafunzo mengine ambayo hayajabainishwa katika ngazi zilizotajwa.

j. **Shilingi bilioni 384** ni kwa ajili ya **Hifadhi ya Jamii** (Inajumuisha; huduma kwa walemavu, wazee, waathirika, familia na watoto, ukosefu wa ajira).




## *Mipango na Matumizi ya Mwaka 2017/18 Kisekta*


Kufuatana na Majukumu ya Serikali matumizi yamepangwa kutekeleza mipango, programu, miradi na shughuli kwenye sekta mbalimbali. Baadhi yake zimeelekezwa hapa chini kwa muhtasari kama ifuatavyo:

### Viwanda

Katika juhudi za kusaidia Mkakati wa kujenga uchumi wa viwanda, Serikali itaendelea kutoa vivutio ili kukuza ujenzi wa viwanda. Pamoja na mambo mengine, Serikali itatumia ipasavyo rasilimali zilizopo na kutumia malighafi zinazozalishwa ndani. Hivyo, itasaidia kuwa ni kichocheo cha sekta zingine ikiwemo kilimo, fedha, mifugo, misitu,

kilimo cha mboga na matunda, na sekta zingine zinazohusiana. Kadhalika, Serikali imetenga fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi maalum ikiwa ni pamoja na miradi ya kielelezo kwa lengo la kuweka msingi kwa uchumi wa viwanda. Katika kutekeleza agenda ya uchumi wa viwanda, SIDO imepewa majukumu yote ili kurahisisha mchakato wa kuanzisha viwanda vidogo nchini. Baadhi ya matumizi kwenye sekta ya viwanda ni pamoja na:

a) **Shilingi bilioni 12. 94** kwa ajili ya uendelezaji wa eneo la viwanda TAMCO Kibaha ikiwa ni pamoja viwanda vya nguo na uunganishaji wa matrekta.
b) **Shilingi bilioni 10.5** kwa ajili ya kendeleza klasta ya viwanda hususani vya ngozi na mazao yatokanayo na ngozi Dodoma.
c) **Shilingi bilioni 14.1** kwa ajili ya kuendeleza viwanda vidogo, biashara ndogo na ujasiriamali ambayo inahusisha ujenzi wa maeneo ya viwanda katika mikoa ya Dodoma, Geita, Kagera, Katavi, Manyara, Mtwara, Njombe, na Simiyu; na
d) **Shilingi bilioni 6.5** ili kuboresha na kuwezesha utafiti wa maendeleo ya utafiti wa viwanda kwenye taasisi za TIRDO, TEMDO, na CAMARTEC.
e) **Shilingi bilioni 2.070** kwa ajili ya kufufua kiwanda cha General Tyre na mashamba ya mpira pamoja na Mradi wa magadi bonde la Engaruka;




## Kilimo, Mifugo na Uvuvi

Mkazo utakua ni kuchochea uwekezaji kwenye sekta ya kilimo (ikiwa ni pamoja na mifugo na uvuvi) ili kuongeza tija na kipato kwa wakulima na wote walioajiriwa kwenye

sekta hii. Hivyo, bajeti imetengwa kuboresha mazao ya kilimo ikilenga zaidi kuongeza thamani ya mazao na kuzifanya shughuli kuwa za kisasa zaidi kwa kutoa pembejeo, huduma za ugani na mafunzo. Sekta ya kilimo imetengewa bajeti ya **shilingi bilioni 1,044** na dondoo za matumizi ni kama ifuatavyo:

a) **Shilingi bilioni 377.5** kwa ajili ya uendelezaji wa utafiti na huduma za ugani.
b) **Shilingi bilioni 308.2** kwa ajili ya uendelezaji wa miundombinu ya kilimo.





c) **Shilingi bilioni 98.9** kwa ajili ya miradi mikubwa ya kilimo cha kibiashara na kusaidia maendeleo ya viwanda.
d) **Shilingi bilioni 81.0** kwa ajili ya hifadhi na usalama wa chakula na lishe ikiwemo ununuzi wa nafaka tani 305,424. Shilingi bilioni 49.4 kwa ajili ya uendelezaji wa miundo mbinu ya masoko na huduma ndogo za kifedha hususani maeneo ya vijijini,
e) **Shilingi 46.8 bilioni** kwa ajili ya uendelezaji wa mifugo na uvuvi.
f) **Shilingi bilioni 43.8** kwa ajili ya pembejeo za kilimo ili kurahisisha upatikanaji wa mbolea, matrekta, vifaa vya umwagiliaji na mbegu bora.
g) **Shilingi 38.8 bilioni** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya umwagiliaji kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini.

## Usafirishaji

Bajeti ya sekta ya usafiri ina lengo la kuharakisha maendeleo ya viwanda na kukuza uchumi kwa kuwekeza kwenye miundombinu ya kiuchumi hususan barabara, reli, viwanja vya ndege, bandari na mawasiliano. Serikali imetenga **shilingi bilioni 5,541.3** kwa ajili ya sekta ya usafiri, ambapo matumizi muhimu ni kama ifuatavyo:

a) **Shilingi bilioni 917.548** kwa ajili ya ujenzi, matengenezo na ukarabati wa barabara kuu za mikoa na wilaya kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara;
b) **Shilingi bilioni 1,052.0** kwa ajili ya ujenzi wa km 778.4 za barabara za lami nchi nzima, ukarabati na matengenezo ya km 150 za barabara za lami, uboreshaji wa km 465.5 za barabara za mikoa kiwango cha changarawe na ujenzi wa madaraja 25;
c) **Shilingi bilioni 176.368** kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya viwanja vya ndege;
d) **Shilingi bilioni 500.00** kwa ajili ya kufufua Shirika la Ndege la Taifa (ATCL);
e) **Shilingi bilioni 900.00** kwa ajili ya ujenzi wa reli mpya ya Kati kwa kiwango cha *Standard Gauge* (Dar es Salaam - Tabora - Isaka - Mwanza), ulipaji wa fidia ya eneo la Buhongwa (Mwanza), upatikanaji wa ardhi eneo la Ihumwa (Dodoma) na maeneo ya Mpiji na Soga (Pwani);
f) **Shilingi bilioni 218.569** kwa ajili ya kujenga reli mpya kwa kiwango cha *standard gauge* pamoja na kukarabati reli iliyopo kwa kutumia **Mfuko wa Reli**;
g) **Shilingi bilioni 251.0** kwa ajili ya kukarabati Reli ya Kati iliyopo kati ya Dar es Salaam na Isaka, kuboresha njia za reli zilizopo bandarini pamoja na kukarabati madaraja na makaravati.
h) **Shilingi bilioni 24,496** kwa ajili ya ujenzi wa meli mpya ya abiria Ziwa Victoria pamoja na ukarabati na matengenezo ya meli zilizopo Ziwa Tanganyika, Victoria na Nyasa;
i) **Shilingi bilioni 26.0** kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA);
j) **Shilingi bilioni 30.8** (kupitia TRL) kwa ajili ya ununuzi na ukarabati wa vichwa na mabehewa ya treni;




k) **Shilingi bilioni 487.281** (kupitia TPA) kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kupakia na kupakua mizigo bandarini na uboreshaji wa Bandari za Dar es Salaam, Tanga, Mtwara na bandari za Ziwa Victoria, Tanganyika na Nyasa; na
l) **Shilingi bilioni 14.00** kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu muhimu ya TEHAMA, udhibiti na uratibu wa Mfumo wa Taifa wa TEHAMA na matumizi yake.

## Nishati na Madini

Mkazo mkubwa ni pamoja na: Kuimarisha ufuajii, usafirishaji na usambazaji wa nishati; Kuimarisha ufuatiliaji wa usalama, mazingira na uzalishaji wa madini kwa wachimbaji wadogo; na Kuboresha ukusanyaji wa mapato ya Serikali yanayotokana na gesi asilia na madini; Fedha zilizotengwa kwenye sekta ya nishati na madini zinafikia jumla ya **shilingi bilioni 998.3.** Sehemu kubwa ya fedha hizi zimeelekezwa kwenye miradi ya kipaumbele ya sekta kama ifuatavyo:

a) **Shilingi bilioni 499.1** zimetengwa kwa Wakala wa Nishati ya Umeme Vijijini kupitia Mfuko wa Umeme Vijijini ili kutekeleza miradi ya awamu ya III ya usambazaji wa umeme vijijini.
b) **Shilingi bilioni 7.7** kwa ajili ya ujenzi wa mitambo ya kufua umeme wa maji katika maeneo ya Rusumo, Malagarasi na Kakono;
c) **Shilingi bilioni 11.0** bilioni kwa ajili ya ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kV 220 Makambako – Songea;
d) **Shilingi bilioni 39.6** kwa ajili ya kuendeleza Gridi ya Kaskazini-Magharibi kwa ujenzi wa njia ya Umeme msongo wa kV 400;

e) **Shilingi bilioni 91.8** kwa ajili ya ujenzi wa njia ya Umeme ya msongo wa kV 400 gridi ya Kaskazini - Mashariki (Dar - Tanga - Arusha);
f) **Shilingi bilioni 10.0** kwa ajili ya kuendeleza Mgodi wa Makaa ya Mawe Kiwira pamoja na ujenzi wa Mtambo wa Kufua Umeme wa MW 200;
g) **Shilingi bilioni 8.9** kwa ajili ya uendelezaji wa sekta ndogo ya madini ikijumuisha uanzishaji wa kituo cha maonesho ya madini;
h) **Shilingi bilioni 10. 0** ajili ya uendelezaji wa ujenzi wa mtambo wa kufua umeme wa MW 240 (Kinyerezi II) kwa kutumia gesi asilia;
i) **Shilingi bilioni 90.0** ajili ya upanuzi wa Mtambo wa Kufua Umeme wa MW 185 (Kinyerezi I);
j) **Shilingi bilioni 26.8** kwa ajili ya kujenga uwezo wa kisekta na kitaasisi katika sekta ya nishati na madini;
k) **Shilingi bilioni 35.5** kwa ajili ya uibuaji na uendelezaji wa nishati mbadala na nishati jadidifu;
l) **Shilingi bilioni 18.1** kwa ajili ya kuongeza usambazaji wa umeme kwa kujenga njia ya usafirishaji wa umeme kutoka Ubungo – Kipawa– Gongo la Mboto – Kurasini;
m) **Shilingi bilioni 12.2** kwa ajili ya kuongeza uwezo wa TANESCO katika uanzishajii wa miradi ya umeme; na
n) **Shilingi bilioni 76.1** kwa ajili ya uendelezaji wa sekta ndogo ya mafuta ikijumuisha ujenzi wa Bomba za Kusafirisha Mafuta Ghafi kutoka Kabaale (Uganda) hadi Tanga.

## Elimu

Bajeti ya Elimu kwa kiasi kikubwa inalenga: Kutekeleza elimu ya msingi na sekondari bila malipo; Kujenga na kukarabati miundombinu ya elimu; Kuinua ubora wa elimu na kujenga ujuzi stahiki katika ngazi zote za elimu; Kutoa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu; Kuimarisha utafiti na matumizi ya sayansi na teknolojia katika kuchochea maendeleo ya kiuchumi. Katika mwaka 2017/18, Serikali imetenga **shilingi bilioni 4,706.3** kwa ajili ya sekta ya elimu. Dondoo muhimu katika matumizi ni kama ifuatavyo:

a) **Shilingi bilioni 201.6** kwa ajili ya kutekeleza mpango wa elimu bila malipo;
b) **Shilingi bilioni 114.1** kwa ajili ya uendeshaji wa mitihani ya kitaifa ya shule za msingi, sekondari na vyuo vya ualimu nchi nzima;
c) **Shilingi bilioni 1,336.6** kwa ajili ya mafunzo ya ufundi na Ufundi Stadi ambapo zitatumika kusaidia vyuo vya Ufundi Stadi nchi nzima ;

d) **Shilingi bilioni 68.7** kwa ajili ya matengenezo na uendeshaji wa vyuo vikuu na Tume ya sayansi na Teknolojia.
e) **Shilingi bilioni 427.5** zitatumika kutoa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu;




f) **Shilingi bilioni 106.6** zitatumika kuboresha elimu ikiwa ni pamoja na ukarabati wa vyuo vya walimu na kuimarisha ukaguzi.

## Afya

Bajeti ya Sekta ya Afya inalenga kutoa huduma bora za afya kwa wananchi wote. Serikali imetenga bajeti ya Sh bilioni 2,222.3 kwa ajili ya sekta ya afya. Matumizi muhimu kwa mwaka 2017/18 katika sekta hii ni pamoja na:

c) **Shilingi bilioni 12.1** kwa ajili ya kupunguza vifo vya akina mama wakati wa kujifungua. Fedha hizo zitatumika kuboresha miundombinu ya kutolea huduma za afya katika maeneo yaliyobainika kuwa na changamoto za utoaji huduma.
d) **Shilingi bilioni 14.5** kwa ajili ununuzi PET SCAN, itakayotumika kufanya uchunguzi wa saratani kwa ufanisi zaidi katika Taasisi ya Saratani ya Ocean Road.
e) **Shilingi bilioni 236,41** kwa ajili ya ununuzi, uhifadhi na usambazaji wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi nchini kote.
f) **Shilingi bilioni 3.89** kwa ajili ya kuimarisha vyuo vya mafunzo ya afya.
g) **Shilingi bilioni 22,93** wa ajili ya posho za madaktari walio katika mafunzo kwa vitendo.



h) **Shilingi bilioni 364.62** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya huduma za kinga ikiwa ni pamoja na udhibiti wa magonjwa ya kuambukiza, Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Ukimwi, pamoja naMpango wa Taifa wa Kudhibiti Kifua Kikuu na Ukoma.
i) **Shilingi bilioni 5** kwa ajili ya matibabu ya matibabu nje ya nchi, kwa ajili ya wagonjwa waliopata rufaa ya matibabu maalum nje ya nchi.

## Maji

Pamoja na mambo mengine, bajeti ya sekta ya maji inalenga kuboresha usimamizi na maendeleo, kusimamia rasilimali za maji nchini, usimamizi wa ubora wa maji, kuboresha upatikanaji wa huduma ya maji na usafi na pia kuboresha miundombinu ya umwagiliaji. Bajeti iliyopangwa kwa mwaka 2017/18 ni **shilingi bilioni 747.91**, ambapo matumizi muhimu yameoneshwa kama ifuatavyo:

a) **Shilingi bilioni 237.8** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji vijijini.
b) **Shilingi bilioni 91.0** kwa ajili ya kuboresha huduma za maji mijini.
c) **Shilingi bilioni 62.5** kwa ajili ya kuboresha huduma za maji na usafi jijini Dar es Salaam;
d) **Shilingi bilioni 37.0** kwa ajili ya kutekeleza mradi wa maji Same – Mwanga – Korogwe;
e) **Shilingi bilioni 21.0** kwa ajili ya kutekeleza mradi wa maji Kahama – Nzega – Igunga- Tabora;
f) **Shilingi bilioni 19.5** kwa ajili ya kukarabati na kupanua mtandao wa kupitisha maji safi na majitaka Jijini Arusha;




g) **Shilingi bilioni 12.0** kwa ajili ya jenzi wa mtandao wa majisafi katika Miji ya Babati, Mtwara, Kigoma, Sumbawanga, Lindi na Morogoro;
h) **Shilingi bilioini 10.5** kwa ajili ya mradi wa ujenzi na ukarabati wa mabwawa pamoja na upanuzi wa miundombinu ya maji kutoka kwenye mabwawa;
i) **Shilingi bilioni 7.9** kwa ajili ya kupanua mtandao wa majitaka mjini Mwanza, Bukoba na Musoma; na Kujenga mtandao wa majisafi katika Miji ya Lamadi, Misungwi na Magu;
j) **Shilingi bilioni 7.52** kwa ajili ya upanuzi wa miundombinu ya maji vijijini;
k) **Shilingi bilioni 5.0** kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya kusambaza maji katika mikoa ya Dodoma, Shinyanga, Singida, Pwani, Manyara, Katavi, Lindi, Songwe na Simiyu;
l) **Shilingi bilioni 5.0** kwa ajili ya kuboresha huduma za maji katika makao makuu ya Mikoa mipya; na
m) **Shilingi bilioni 4.**1 kwa ajili ya kutekeleza mradi wa maji Kigoma.

## Hifadhi ya Jamii

Serikali itaendelea kuwezesha makundi maalum kupata huduma za msingi na kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo. Pia, itaendelea kuwezesha kiuchumi na kuweka

mazingira endelevu ya fursa za ajira. **Shilingi bilioni 384.2** zimetengwa kushughulikia masuala ya hifadhi ya jamii na kiasi kikubwa kimegawanywa kama ifuatavyo:

a) **Shilingi bilioni 68.7** ambayo ni asilimia 10 ya mapato yanayokusanywa kutoka vyanzo vya Halmashauri, zimetengwa kwa ajili ya makundi ya vijana na wanawake katika ngazi ya Serikali za Mitaa.
b) **Shilingi bilioni 16** kwa ajili ya programu mahsusi ambapo Shilingi bilioni 15.0 ni kwa ajili ya kuwezesha Programu ya Kukuza Ujuzi Nchini na Kuongeza Fursa za Ajira na Shilingi bilioni 1.0 kwa ajili ya Mfuko wa Mradi wa Maendeleo wa Vijana.
c) **Shilingi bilioni 60** kuwawezesha vikundi vidogo vidogo vya kiuchumi vijijini ambapo kila kijiji kitapata shilingi milioni 50 kwa awamu kupitia mfuko unaojiendesha.
d) Serikali itatoa mikopo yenye thamani ya **Shilingi bilioni 12**, kupitia Benki ya Wanawake (TWB), kwa wanawake wajasiriamali 9,650 jijini Dar es Salaam, Mbeya, Njombe, Iringa, Dodoma, Ruvuma, Pwani na Mwanza.
e) **Shilingi bilioni 115** zimetengwa ili kuboresha huduma ya wazee (chakula, malazi na huduma ya matibabu) nchini kote na kukomesha mauaji ya wazee.

## NYARAKA REJEA ZA BAJETI

Ifuatayo ni orodha ya nyaraka zinazochapishwa na Serikali na kutumika kama chanzo cha taarifa za kuandaa bajeti:

a) Dira ya Maendeleo ya Tanzania, 2025 pamoja na Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano;
b) Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi 2015 – 2020;
c) Mfumo wa Sera za Uchumi Jumla: Unatoa taarifa juu ya sera za bajeti na maboresho;
d) Mkakati wa Taifa wa Madeni;
e) Mkakati wa Pamoja wa Misaada Tanzania;
f) Mipango ya Muda wa Kati na Randama ya Mfumo wa Matumizi wa Muda wa Kati ya mwaka 2017/18;
g) Hotuba ya Bajeti za Mawaziri 2017/18;
h) Hotuba ya Hali ya Uchumi ya mwaka 2017/18;
i) Hotuba ya Bajeti ya Serikali ya mwaka 2017/18;
j) Sheria ya Fedha ya Mwaka 2017;

k) Sheria ya Matumizi ya mwaka 2017;
l) Hali ya Uchumi;
m) Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2017/18 (Juzuu Na. I – hadi IV).

Ili kupata baadhi ya nyaraka hizi na matoleo ya nyuma ya vijitabu vya Bajeti Toleo la Mwananchi, uneweza kutembelea mitandao ya:

- Wizara ya Fedha na Mipango (www.mof.go.tz)
- Tume ya Mipango (www.mipango.go.tz)
- Policy Forum (www.policyforum.or.tz)

**…….………(Kwa maoni zaidi kata ukurasa huu)………………….**

Je, una mawazo gani, maswali, hisia (unafikiria nini), au una maoni gani kuhusu bajeti hii?

------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

--------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

Je, unahitaji taarifa zaidi ya hii iliyotolewa katika kijitabu hiki? □NDIYO □HAPANA

Kama ndiyo Je, unahitaji taarifa ya aina gani?

------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

-----------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

Je kuna kitu kingine zaidi ambacho ungehitaji sisi tukijue?

------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

-----------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

Je, kijitabu hiki kilikusaidia? □ ndiyo □ hapana □ kiasi Fulani

Je kijitabu hiki kilikuwa rahisi kusoma na kueleweka? □ ndiyo □ hapana □ kiasi fulani

**Tuma au fikisha sehemu hii**
Wizara ya Fedha na Mipango,
Idara ya Bajeti ya Serikali,
***18 Mtaa wa Kikwete Street***
***40468 Dodoma***
***S.L.P 2802, Dodoma***
Au tuma kwa njia ya barua pepe kwa: ps@mof.go.tz

## Je, Utafanya nini na Taarifa hii?

Bajeti ya Serikali ni taswira muhimu ya sura halisi ya kile ambacho Serikali inapanga kufanya kwa mwaka husika. Ukitaka kujua fedha yako ya kodi inakoenda, kama kuna mpango wa kuboresha elimu, afya, n.k katika eneo lako, unaweza kuangalia namna na jinsi ambavyo mgawanyo wa fedha unafanyika, hususan kwa ajili ya maendeleo. Kijitabu hiki kinajaribu kutoa muhtasari wa baadhi ya taarifa hizi kwa namna iliyo rahisi kadiri iwezekanavyo. Hata hivyo unaweza kupata taarifa zaidi kuhusu mchakato wa uandaaji wa bajeti kutoka katika vyanzo vifuatavyo:

- Nyaraka zenye taarifa za bajeti ya Tanzania (***angalia orodha ya nyaraka za rejea***) na hasa, vitabu vinne vya bajeti ya taifa mbavyo vinapatikana katika Wizara ya Fedha (yaani Juzuu Na. I –hadi IV) .
- Wizara ya Fedha na Mipango S.L.P 2802, Dodoma (tovuti http://www.mof.go.tz)
- Ofisi za Halmashauri na/au Maofisa katika eneo lako kama Mwenyekiti Mtendaji wa Kijiji au
- Policy Forum, S.L.P. 38486, Dar es Salaam.

Kumbuka kwamba ni haki yako kujua bajeti hii na taarifa nyingine zinazohusiana na bajeti ya Taifa. Ongea na Viongozi wako kuhusu taarifa hizi na washirikishe watu wengine katika jamii unayoishi nayo.